# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI 31 JANUARI 2025

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, FRANCO ATILYO**

Kwa wiki inayoishia tarehe 31 January 2025, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yaliopungua kwa asilimia 13.01 kutoka TZS 7.95 bilioni hadi TZS 6.9 bilioni. Kiasi cha hisa zilizouzwa kilipungua pia kutoka hisa milioni 7.55 hadi hisa milioni 6.95 sawa na asilimia 7.94.

Jumla ya Mtaji wa Soko ulipungua kwa asilimia 0.63, kutoka TZS 18.6 trilioni hadi trilioni 18.5. Mtaji wa Soko la Ndani uliongezeka kwa asilimia 1.62, hadi TZS 12.57 trilioni kutoka TZS 12.37 trilioni kutokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za AFRIPRISE,CRDB, na NMB.

CRDB imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 4.26 bilioni, ambayo ni 61.64% ya mauzo yote ikifuatiwa na NMB kwa asilimia 33.16 ya mauzo yote.

Kuhusu bei, hisa za AFRIPRISE ziliongezeka kwa TZS 5 wakati za CRDB ziliongezeka kwa TZS 20 huku za NMB zikiongezeka kwa TZS 250.

CRDB iliongoza kwa idadi ya kubwa ya hisa zilizouzwa kwa asilimia 89 sawa na hisa milioni 6.2 ikifuatiwa na NMB kwa asilimia 6. Jumla ya hisa milioni 2.43 za CRDB, TCC na NMB ziliuzwa kupitia kaunta ya makubaliano ya kabla huku wawekezaji wa nje wakiongezeka kiasi wiki hii. Tunatarajia kuongezeka kwa mwitikio utakaoakisi kwenye mauzo ya hisa na bei kwa wiki zijazo.

Katika wiki kulikuwa na miamala 79 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 109.6 bilioni.

Mnada wa dhamana za Serikali za muda mfupi uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 29 Januari 2025, ulisajili zabuni 98 ambapo zabuni 86 zilifanikiwa na kukusanya kiasi cha TZS 17.48 bilioni.

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA JANUARI 31, 2025. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI FRANCO ATILYO**